

WASINDIKAJI WA MCHELE WAJENGWEA UWEZO WA KUHUDUMIA MASOKO YA NDANI NA NJE, DESEMBA, 2021

1.0 HALI YA SEKTA YA MCHELE

Mchele ni miongoni mwa mazao ambayo hunazalishwa kwa wingi nchini baada ya Mazao ya mahindi. Uzalishaji wa mpunga unakadiriwa kuwa zaidi ya tani milioni tano na laki mbili (milioni 5.2) ambapo unapelekea kupatikana kwa mchele unakadiriwa kuwa zaidi ya tani milioni Mbili na laki mbili (milioni 2.2) Kipindi cha Mwaka 2020/2021 kumekuwa na ongezeko la uzalishaji ikilinganishwa na mahitaji ambapo zaidi ya tani Milioni moja na laki tano (Milioni 1.5) na hivyo kuonesha uhitaji wa kuboresha zaidi sekta hiyo kibiashara ili kuwa na bidhaa zinazokidhi ushindani wa Masoko ya Ndani na Nje.

2.0 MAELEZO YA MRADI

Kutokana na umuhimu wa Sekta ya mchele na mchango wake kwenye Lishe, Ajira, Kipato na ukuaji wa Viwanda, Baraza la Mchele Tanzania(RCT) chini ya ufadhili wa Taasisi mbalimbali na kwa kushirikiana na TanTrade waliendesha semina na Ziara za mafunzo maeneo ya usindikaji (SMEs extension Visit) kwa Wazalishaji wa Mpunga na Mchele ili kuwawezesha kuboresha mazao yao na kuwa na mikakati endelevu ya kuyafikia Masoko.

Wadau muhimu walionufaika na mafunzo ya Mradi husika ni pamoja na Wasindikaji wa Mchele wa Mtibwa Wilayani Mvomero, Mkoani Morogoro Tarehe 15.11.2021, Kilorice/WAMI Valley Wilayani Kilosa tarehe 17.11.2021 na Wasindikaji wa Wilaya ya Kilombero katika halmashauri za Ifakara na Mlimba Mkoani Morogoro.

Miradi kama hiyo imewahi kutekelezwa pia katika maeneo ya usindikaji kwa kipindi cha Mwezi Mei 2021 kwa wasindikaji wa Magugu-Manyara, Arumeru-Arusha na maeneo ya Kivulini, Kileo na Kirya katika Wilaya ya Mwanza Mkoani Kilimanjaro, mnamo tarehe 28.05.2021.

Aidha, Mafunzo kama hayo ambayo yanalenga kujenga uwezo na kuimarisha Biashara za Nafaka ya Mchele, yalifanyika Mikoa Nyanda za Juu Kusini katika maeneo ya Mbarali Mkaoni Mbeya, Ruaha Mkoani Iringa na pia Kilombero, Ifakara na Malinyi kwa Mkoa wa Morogoro na baadae Kahama Mkoani Shinyanga kwa kipindi cha Februari hadi Mei 2021. Program hizi kwa kipindi cha 2020/2021 imeweza kuwanufaisha Wasindikaji na Wafanyabiashara wasiopungua 250 (SMEs) katika maeneo yaliyotajwa.

(Picha: Washauri Wataalam wa RCT na TanTrade wakiwa na Viongozi wa Kilorice katika eneo la kilosa Msalabani baada ya kutoa ushauri kuhusu Menejimenti ya kampuni na Masoko)



3.0 MAFUNZO NA USHAURI

- ✓ Wasindikaji walielimishwa kuhusu mbinu bora za ufungashaji wenye kuzingatia ujazo, uwekaji wa chapa na rajamu (Branding) kama sehemu ya mkakati wa kufanikisha masoko;
- ✓ Ushauri kuhusu menejimenti ya kampuni za mchele;


4.0 MABADILIKO CHANYA

- Wasindikaji wameanza kufuata ushauri wa Wataalam ambapo baadhi wameboresha menejimenti zao kwa kuanziasha vitengo vya kimasoko na Lojistiki ambavyo havikwepo;
- Utaratibu wa kufungasha na kutia rajamu umeanza kufanyika tofauti na awali

- ✓ Ushauri wa kupata taarifa za mwenendo wa masoko ya mchele ili kuwawezesha Wazaliashaji kujipanga na kuzingatia mahitaji ya masoko;
- ✓ kuimarisha vyama vyao vya ushirika ili kupunguza gharama zitakazolazimisha kuuza mchele bei ya juu kuliko uhalisia wa masoko.
- ✓ Wadau wameshauriwa pia namna ya kuongeza uzalishaji kwa matumizi ya Mbegu bora na Viwatilifu kwa muda sahihi;Uvunaji, ukaushaji na uhifadhi mzuri wa mpunga ikiwa ni pamoja na uchakataji wenye kuzingatia viwango ili kuweza kupata mchele mzuri;

wengi walitumia zaidi magunia;

- Uwekaji wa madaraja katika mchele umeongezeka.
- Baadhi ya Makampuni tayari yamepata mahitaji ya Masoko ya Nje ikiwemo eneo la Masoko ya SADC na Afrika Mashariki (EAC).



Picha: Majadiliano ya Wataalam na Menejimenti ya Kiwanda cha KTC-Mlimba-Kilombero, tarehe 17.11.2021

Kufahamu namna unavyoweza kupata huduma za Kibiashara za TanTrade au Kitengo cha SMEs Tembelea Tovuti www.tantrade.go.tz au ujumbe wa Barua pepe: info@tantrade.go.tz